# Learning by Ear 2011/2012 – Corruption – The Elephant in the Room

## Episode 07 – "Crooks, Detectives, and a New Politician"

**Text: Victoria Averill**

**Editing: Johannes Beck, Friederike Müller, Pendo Paul**

**Proofreading: Charlotte Collins, Pendo Paul**

**Kisuahli: Eric Ponda**

Intro & Outro:

- NARRATOR

Scene 1:

- Sylvia (FEMALE, 19)
- Jeffrey (MALE, 58)
- Answering machine (FEMALE, 30)
- Anonymous (MALE, 50)
- NARRATOR

Scene 2:

- Lydia (FEMALE, 16)
- Tekla (FEMALE, 16)
- Miss Tatu (FEMALE, 43)

## Intro:

### 0. Narrator:

Hujambo na karibu katika makala haya ya saba katika mfululizo wa vipindi vya Learning By Ear “**Noa Bongo Jenga maisha yako**”. Tukiwa bado kwenye ule mchezo wa redio kuhusu ufisadi, kwa jina “**Tembo Nyumbani**” Katika mfululizo wa vipindi hivi kumi, tunafuatilia maisha ya familia ya Bwana Odhiambo na Rafiki yao Jeffrey katika kupambana na ufisadi. Katika kipindi kilichotangulia, Lydia Odhiambo na rafiki yake Tekla wanagundua kwamba mwalimu wao anapokea rushwa. Na sasa wanamtaka Jeffrey Thiongo na shirika lake la “**Komesha Ufisadi Sasa**” kuchunguza kashfa hii. Lakini wanahitaji ushahidi wa kutosha kufanikisha uchunguzi huu. Kwa upande mwengine; babake Lydia, Alfayo Odhiambo anaandikisha taarifa ya ushahidi kuhusu sakata linaloikumba sekta ya nishati. Katika kipindi cha leo kuhusu “**Walaghai, Wapelelezi na Wanasiasa wapya**”, Jeffrey anatafakari hatua ya kujitosa katika ulingo wa sisasa kugombea kiti cha ubunge

huku naye Lydia na rafiki yake Tekla wanageuka kuwa majasusi. Moja kwa moja tunaanza makala haya ofisini kwa Jeffrey katika shirika lake la ‘**Komesha Ufisadi Sasa**’.

## Scene One:

**1. Atmo:** **Office sounds**

**2. SFX:** **Door opening**

**3. Jeffrey:** **(shouting)** Sylvia, tafadhali pokea huo ujumbe kutoka kwa mashine yetu. Nina shughuli kidogo hapa ya kupitia hizi stakabadhi. Kwa hakika tumepata kuangaziwa sana katika vyombo vya habari. Nadhani mahojiano tuliyofanya kupitia Redio Easy FM yatakuwa hewani mwendo wa saa tano asubuhi. Tusisahau kusikiliza....

**4. Sylvia:** Sawa natayarisha kahawa... Ungependa kikombe cha kahawa?

**5. Jeffrey:** Oh, sawa. Lakini maziwa pekee tafadhali.

**6. Sylvia:** Ooooh tuna ujumbe mwingi sana hapa!

**7. SFX:** **Answering machine beep**

**8. Answering Machine:** Jumla tumepokea zaidi ya ujumbe 10, ujumbe wa kwanza umetumwa saaaa... mbili na dakika 14 asubuhi.

**9. Anonymous: (recorded on answering machine)**

”*Tunafahamu kwamba umepata kuungwa mkono sana katika sehemu nyingi za nchi. Lakini tunakutahadharisha kuwa mambo si sawa katika sehemu nyingine. Kwa hivyo, usithubutu. Futa*

*kabisa katika akili yako ndoto ya kuendelea na uchunguzi wako na kisha ufunge hizo ofisi za shirika lenu. Unakumbuka yule mtu wa mwisho aliyejaribu kufuatilia mambo yetu...?Nini kilichomtokea?. Alikufa kwenye ajali ya barabarani. Hatutaki kuona haya yakitokea kwako... au unataka tukuonyeshe Jefrrey?*

**10. SFX:** **Answering machine beep**

**11. Answering Machine:** Ujumbe mwengine, umetumwa saaa... 3:11-- **(stopped)**

**12. Sylvia:** Oh Mungu wangu umesikia hiyo Jeffrey?

**13. Jeffrey:** Ndio nimesikia. **(worried)** Lakini si mara ya kwanza kupokea ujumbe na vitisho hivyo.

**14. Sylvia:** Nini? Na mbona hujaniambia.

**15. Jeffrey:** Hapana ni kuhusu ujumbe huo huo. Nadhani ni mara ya tatu sasa. Wiki iliyopita watu wasiojulikana walibandika karatasi yenye ujumbe kama huo kwenye kioo cha gari langu. Na nadhani ni watu hao hao tu waliokuja nyumbani kangu na kuandika ujumbe kwenye kioo cha bafuni mwangu – Na ujumbe ni sawa tu na huu uliotumwa kwenye mashine.

**16. Sylvia:** Jeffrey! Kwani huogopi? Nadhani tungepunguza kasi kidogo... Kweli kuna haja ya kuhatarisha maisha yetu au la?

**17. Jeffrey:** Nimekuwa nikilifikiria sana jambo hili Sylvia. Lakini sasa nitafanya nini? Moyo wangu umejikita katika suala hili. Na tayari nimejua mengi sana. Hata

kama sitafunga shirika langu bado kuna uwezekano wa kuniua ili kuhakikisha wanaufunga mdomo wangu,.. kwa hivyo sina jinsi!

**18. Sylvia:** Ukisema hivyo nakuelewa. Kwa hivyo tufanye nini?

**19. Jeffrey:** Nimekuwa nikifiria kuhusu swali nililoulizwa na waandishi wa habari siku ile ya mahojiano.

**20. Sylvia:** Kuhusu kugombea ubunge?

**21. Jeffrey:** Ndio. Nafikiri wakati umefika. Kwa kuzingatia vitisho hivi bora tu nijiimarishe kwa kukuza hadhi yangu badala ya kuporomoka.

**22. Sylvia:** Naelewa unachomaanisha. Ukijitokeza zaidi hadharani, itakuwa vigumu kwa maadui wako

kuendelea na vitisho au hata kufikiria kukufanyia jambo baya.

**23. Jeffrey:** Ni kweli na pindi nitakapoingia bungeni labda nitapata kipande cha kula keki hii inayotokana na ufisadi.… **(laughter)** Usijali nakutania tu! Lakini kumbuka wanasiasa wengi huwa na mawazo haya wanapogombea ubunge.. ! Kwanza wanaahidi kukomesha kabisa ufisadi, kisha wanapoingia bungeni wananyakua kila kitu. Mara nyingine ni vigumu sana kuwashawishi wapiga kura kwamba mimi nitakuwa tofauti – kwamba nimejitolea kumaliza ufisadi.

**24. Sylvia:** Lakini kugombea ubunge… Ni kweli unataka kujiingiza katika siasa? Kwamba unaweza kufanya mambo tofauti?

**25. Jeffrey:** Ndio…na natumai naweza kuwashawishi watu kwamba nitajitolea kuwapa huduma wanazozihitaji. Kwamba, kweli nataka kuchukua hatua!

**26. Sylvia:** Kwa kuzingatia sifa zako na kazi unayofanya kwa sasa hivi katika kumaliza ufisadi, nadhani watu watakukubali na kuwa na imani nawe.
**(convinced)** Watakuunga mkono, Jeffrey!

**27. Jeffrey:** Nafikiri …Afadhali nijaribu safari hii. Utaniunga mkono Sylvia? Endapo nitafaulu kuingia bungeni, nadhani naweza kubadilisha utaratibu na mfumo ulioko sasa. Najua haitakuwa rahisi hasa katika wiki chache za kwanza.. lakini endapo nitaamua kufanya hivyo, basi nitahitaji msada wako!

**28. Sylvia:** Bila shaka. Tujaribu kukupeleka bungeni. Kisha utakua na nafasi nzuri ya kupambana na ufisadi ukiwa huko bungeni.

**End of Scene One**

**29. Narrator:** Pengine Jeffrey alihitajika kuwasilisha ujumbe wa vitisho kwa maofisa wa usalama. Lakini pia maofisa hao wa polisi aidha hawataki au wanashindwa kufanya uchunguzi ... hasa pale kesi inapowahusisha watu wenye uwezo katika jamii. Hata maofisa wa polisi pia hupokea rushwa, na Jeffrey anafahamu yote hayo...Sasa anaamini kwamba ili kupata nguvu za kupambana na ufisadi mtu anahitaji kuingia katikati ya mfumo huo ili kupambana na wanasiasa au wafanyabiashara walaghai. Hapo ndipo utaweza kuleta mabadiliko. Lakini kabla ya kuona jinsi mambo yanavyokwenda, hebu kwanza tuwageukie Tekla

na Lydia kusikia jinsi wanavyoendelea na mipango yao ya kurekodi sauti ya mwalimu wao.

## Scene Two:

**30. Atmo:** **Outside School Ambience, light traffic**

**31. Tekla:** Uko tayari Lydia? Lydia, unajisikiaje sasa? Kila kitu kiko sawa, waya zote ziko sawa? Kitu ambacho sitaki kuona kikitokea ni kifaa cha kunasa sauti kianguke chini au kikose kufanya kazi.

**32. Lydia:** Nadhani tuko tayari. Nadhani kifaa changu hakionekani kwa upande wa nyuma sivyo?

**33. Tekla:** Hebu geuka! Haionekani!

***KW begin***

**34. Lydia:** Sasa tunajua maswali tutakayomuuliza?

**35. Tekla:** Najua. Tutaanza kwa kumuuliza maswali ili moja kwa moja aanze kuzungumzia suala la kupokea rushwa. Lakini ukianza kukasirika -kama unavyofanya mara nyingi! Nitabadilisha mada ya mazungumzo ili asitufukuze ofisini kwake.

**36. Lydia:** Sawa kabisa, kweli wewe ni ofisa wa ujasusi…Lazima twende moja kwa moja kwa swali hilo la kuchukua hongo ili aweze kukiri na kunasa sauti yake mara moja. Lakini akikasirika anaweza kutoka ofisini bila ya kutamka neno hata moja.

***KW end***

**37. Tekla:** Sawa basi. Nadhani tuko tayari. Nitakufungulia mashine yetu… sasa . Sawa twende ndani!

**38. SFX:** **(School) door opens**

**39. SFX:** **Walking in corridor**

**40. SFX:** **Knocking on the door**

**41. Tekla:** Habari mwalimu Tatu, tafadhali nimekuja kuchukua vitu vyangu nilivyosahau asubuhi. Sahamani kwa usumbufu.

**42. Ms Tatu:** Ni sawa, piteni ninyi wasichana. Sasa najiandaa kwa kazi yangu ya muhula ujao.

**43. Lydia:** Muhula ujao … sivyo…? Hapana shaka utakuwa mwaka mzuri na muhimu sana. Na vipi kuhusu maombi ya wanafunzi kujiunga na chuo kikuu... Mimi na Tekla tunahitaji kuimarisha alama zetu mwalimu. Tunahitaji kupata alama nzuri ili kuendelea na masomo yetu katika chuo kikuu.

**44. Ms Tatu:** Kweli mnahitaji kuendelea na masomo yenu katika chuo kikuu. Ni vyema kufanya bidii zaidi masomoni...lakini kama tulivyozungumza wakati tulipokutana, zipo njia nyingine pia.....

**45. Tekla:** Ohh na kweli Mwalimu Tatu..! Tumekuwa tukilifikiria sana suala hili tangu ulipotuelezea. Je, iwapo wazazi wetu wako tayari kukusaidia kidogo kama ulivyosema, haitakuwa hatari?

**46. Ms Tatu:** Hata hakuna hatari kabisa. Na si mimi pekee yangu anayechukua pesa- na tafadhali usiseme ni hongo- kama ulivyotaja mara ya kwanza! Naonekana mhalifu! **(laughs)** Pengine tuseme ni pesa za kuimarisha matokeo. "Au ada maalum kwa usaidizi wa mwalimu"... **(laughs)** Kwanza kabisa walimu katika shule nyingi wakiwemo

walimu wakuu hufurahia sana kupokea pesa hizi ili kuimarisha alama za wanafunzi.

**47. Lydia:** Ni kweli Mwalimu Tatu? Sikuwa na habari. Hebu fikiria, Tekla – kwa miaka mingi wazazi wetu wamekosa fursa hii. **(laughs)**

**48. Ms Tatu:** Nafahamu hilo **(chuckling)**. Bila shaka bidii ndio msingi wa kila jambo. Lakini wakati mwengine sisi walimu tunalipwa mishahara duni sana,...tufanyeje?

***KW Begin***

**49. Tekla:** Kwa hiyo hakuna mwanafunzi anayeweza kusonga mbele kimasomo aidha kujiunga na chuo kikuu au vyuo vingine bila ya wewe au walimu kuchukua pesa kutoka kwa wazazi?

**50. Ms Tatu:** Inawezekana. Mwanafunzi anaweza kufaulu kijiunga na vyuo hivyo lakini itawachukua muda mrefu. Tekla iwapo wazazi wako watanisaidia kidogo basi hapana shaka utakuwa mwanafunzi bora darasani. Na utakuwa katika nafasi nzuri ya kujiunga na chuo kikuu ambapo kila mmoja atajivunia ufanisi wako.

***KW End***

**51. Tekla:** Lakini husikii kujihukumu wakati unapochukua pesa hizi ili kuongeza alama za wanafunzi ambao hawastahili?

**52. Ms Tatu:** Hebu sikiliza, hata kama mimi sitachukua pesa hizi, wazazi watamwendea mwalimu mkuu ambaye hatimaye atanishinikiza kuongeza alama za

mwanafunzi huyo au sivyo ataniachisha kazi mara moja. Sasa kama ni wewe utafanya nini?

**53. Lydia:** Mmmm. Nitafikiria kuhusu suala hili... Ehhh Tekla, tufanye haraka tutakosa basi!

**54. Tekla:** Ni kweli Lydia asante sana Mwalimu Tatu. Kuwa na mwisho mwema wa juma. Sasa tunaondoka!

**55. SFX:** **Two people running out of the classroom**

**56. SFX:** **door slamming**

**End of Scene Two**

**MUSIC (FADE UNDER OUTRO)**

**57. NARRATOR:** Na hadi hapo tunafika mwisho wa makala ya leo kwenye mfululizo wa vipindi vya mchezo wa redio kuhusu ufisadi kwa jina "**Tembo Chumbani**".

Je wasichana wamefaulu kunasa sauti ya Mwalimu wao Bi. Tatu akikiri kula rushwa? Je, naye Jennifer, Bibi ya Alfayo atazipokeaje habari za mumewe kuhusishwa kwenye sakata la nishati?

Ungana nasi kwa kipindi kinachofuata usikie yanayojiri katika hadhithi hii inayozungumzia hali halisi ya maisha. Ukipenda kusikiliza tena makala haya tembelea wavuti wetu wa dw.de/lbe. Au ukiwa na maoni usisite kututumia kupitia Facebook. Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa.